JARIDA KUHUSU |UTALII | UHIFADHI NA MASUALA MBALIMBALI

# TZ&BEYOND

OCTOBER-NOVEMBER 2022 | ISSUE NO 001

Multisectoral magazine



RAIS MWINYI KIONGOZI MBEBA MAONO, UCHUMI WA BULUU KUWA KISIMA CHA
**AJIRA**

## UCHUMI WA BULUU NURU YA
# ZANZIBAR

TSHS.25,000 KSHS.1,300 USHS 40,000
ISSN 2799-225X | LESENI 00000021
www.tz&beyond.co.tz




# BODI YA WAHARIRI


AFISA MTENDAJI MKUU
Emmanuel J. Kakuyu
Cell: 0622411148
ekakuyu@gmail.com

MHARIRI MTENDAJI
Jimmy C. Kiango
Cell: 0787 180 065
jimmy.kiango@tz&beyond.co.tz

MSANIFU KURASA
Felix Jimmy
Cell: 0763 520 319
felix.aloyce@tz&beyond.co.tz

MWANDISHI
Hassan Daud
Cell: 0692 695 889

MWENYEKITI/MLEZI
Dk. Thomas Kashililah
[fclpp, cipm,ChE, AFA]
Cell: 0754 997 645
namkonda@gmail.com



**TZ&BEYOND**
Mbezi Beach Park Building;
Off Bagamoyo Road
P.O. Box 79010, Postcode: 14121
Phone: +255 655 06 38 39
Dar Es Salaam , Tanzania

**MAUZO/MATANGAZO**
Sales Team,TZ&BEYOND
Cell: 0655063839
email: tz1andbeyond@gmail.com





www.tz&beyond.co.tz



# Ulaya NA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR

39 RAIS MWINYI KIONGOZI MBEBA MAONO





07 Uchumi wa Buluu Nuru ya Zanzibar



08 Uchumi wa buluu ni neno tamu





24 Kilimo cha Mwani kuwakomboa wanawake



52 Ulaya na uchumi wa buluu Zanzibar



35 Sekta ya utalii kuimarishwa ili kuvutia wawekezaji



45 Serikali kuimarisha kampuni za mafuta na gesi



33 Miongoni mwa vivutio vya utalii ni pamoja na fukwe



32 Ujenzi wa hoteli za kimataifa



28 Uchumi wa Buluu kisima cha ajira



32 Michezo ya baharini, uzamiaji

## JICHO LA TZ&BEYOND



MHARIRI MTENDAJI: JIMMY C. KIANGO

JARIDA: TZ&BEYOND

COVER STORY: UCHUMI WA BULUU NURU YA ZANZIBAR

# UCHUMI WA BULUU MANUFAA KWA TAIFA

SI ajabu tena kusikia neno Uchumi wa Buluu visiwani Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Hii ina maana ya kuelekeza shughuli zote za uendelezaji na ukuzaji wa uchumi kwenye matumizi bora ya rasilimali zote muhimu za bahari.

Dhana nzima ya Uchumi wa Buluu ni pana ikibeba shughuli zote za msingi zinazofanywa katika bahari ukiwemo uvuvi wa kibiashara na usio wa kibiashara katika kina kirefu na kifupi.

Shughuli za usafirishaji , utafutaji na uchimbaji wa mafuta, utalii, burudani, michezo, ujenzi wa vyombo vya baharini, elimu na utafiti .

Sasa hakuna asiejua kuwa uchumi wa Buluu unafaida kubwa katika ukuzaji wa Uchumi wa nchi yoyote ile iliyozungukwa na bahari, mito au maziwa.

Jicho la TZ&BEYOND na jarida zima linaangazia jitihada na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali kupitia Mamlaka zake kuhakikisha uchumi wa Buluu unakuwa nuru na neema kwa kila Mzanzibari.

Ili kufanikisha hilo tayari mamlaka husika kupitia Serikali kuu imefanya mapitio na kurekebisha baadhi ya Sheria, Kanuni na taratibu mbalimbali zinazotoa fursa kwa wadau mbalimbali kujitokeza katika kuwekeza kupitia bahari kuu ambayo ndio msingi mkuu wa uchumi wa Buluu.

Ili kukuza uchumi wa Buluu inatakiwa kuwekwe mazingira rafiki kwa wavuvi wadogo, wakubwa na hasa kwa wawekezaji wa ndani.

Tayari kuna punguzo la bei za leseni kwa wawekezaji wazawa pamoja na muda wa kutoa leseni ambapo wawekezaji wazawa wataweza kukata leseni kuanzia miezi 3 na kuendelea, huku Mwekezaji mgeni anatakiwa kukata kuanzia miezi 6 na miezi 12, tofauti na ilivyokuwa awali.

Aidha ipo fursa kwa wazawa kuingia ubia na watu wengine wenye uwezo katika kuwekeza katika uvuvi wa bahari Kuu.

Ukweli ni kwamba unapowainua wavuvi wadogo wadogo na kuweka mazingira kwa wawekezaji kuja kuvua katika bahari kuu unakuza uchumi na kipato kupitia bahari.

Tayari mamlaka zimeshafanya utafiti maalumu wa kutambua maeneo mbalimbali ya ukanda wa bahari yenye samaki wa kutosha kwa lengo la kuwaondolea usumbufu na gharama wavuvi.

Jicho la TZ&BEYOND limebaini kuwa Wizara ya Uchumi wa Buluu miandaa mikakati mahsusi ya kukabiliana na changamoto yoyote ile itakayojitokeza wakati Serikali ikitekeleza Sera yake ya kukuza Uchumi kupitia Uchumi wa Buluu.

Wizara imeanza na mkakati wa kukabiliana na changamoto ya uchache wa wataalamu wa kuzihudumia sekta zilizomo katika wizara hiyo.

Tatizo la kukosekanika kwa wataalamu linazikabili nchi nyingi zinazopakana na bahari, hivyo kuna haja ya kuwekwa mikakati itakayoimarisha uchumi kupitia sekta mbali mbali ikiwemo ya uvuvi ambao ndio shughuli mama katika uchumi wa Buluu.

Ili kufikia azma ya Zanzibar kunufaika na uchumi wa buluu, lazima sekta hiyo isimamiwe vyema na kuwekewa mkazo katika vipaumbele vya serikali ya awamu ya nane.

Dhana ya uchumi wa bluu ni mtambuka na inahitaji ushiriki wa kila mmoja wetu, ipo haja ya serikali kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi.

Iwapo changamoto zote zitafanyiwa kazi kimkakati, uchumi wa buluu utakuwa na tija kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Uchumi wa buluu hauishii baharini pekee, badala yake unazalisha fursa zaidi hasa kwenye ujenzi wa bandari ya uvuvi baina ya serikali na sekta binafsi, ujenzi wa sehemu ya kuhifadhia samaki na kujenga kiwanda cha uzalishaji barafu itakayotumika kuhifadhia samaki na mazao mengine ya baharini.

Wakati umefika sasa kwa Wazanzibar kuanza kuvua katika bahari kuu ili kujiongezea tija na faida.

Katika hili la uchumi wa buluu pongezi zinapaswa kuelekezwa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Hussein Ali Mwinyi kwa kuonesha juhudi za kuboresha sekta ya uvuvi kutokana na ukweli kwamba jiografia ya Zanzibar imezungukwa na bahari na wananchi wake wanategemea sana sekta nzima ya Uvuvi.

Jicho la TZ&BEYOND lilipata kusmikia Rais Dk.Hussein Ali Mwinyi akitanabaisha kuwa yeye na Serikali yake dhamira yao ni kujenga Zanzibar mpya kwa kupitia uchumi wa kisasa, Uchumi wa Buluu.

Katika moja ya hotuba zake, Dk Mwinyi Alisema kuwa Uchumi wa Buluu ama uchumi wa bahari unafungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki, ujenzi wa viwanda vya samaki, ukulima wa mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi, matumizi bora ya rasilimali mbali mbali za bahari pamoja na shughuli za utalii wa fukwe na michezo ya baharini.



RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI MHE. DK.HUSSEIN MWINYI AKIAGANA NA MGENI WAKE BALOZI WA KUWAIT NCHINI TANZANIA MHE. MUBARAK MOHAMMED ALSEHAIJAN

# UCHUMI WA BULUU NURU YA ZANZIBAR



# UCHUMI WA BULUU NURU YA ZANZIBAR

DHANA ya uchumi wa buluu ambao ni mkakati wa maendeleo alioibuka nao Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi unakwenda kuwanufaisha Wazanzibari na pengine watanzania kwa ujumla.

Jambo la kufurahisha ni kuwa tayari Wazanzibari wengi wameshaielewa nia na dhamira ya Rais Dkt. Mwinyi, hivyo kwa sasa si ajabu tena kusikia neno Uchumi wa Buluu.

Uchumi wa Buluu unabeba shughuli zote za uendelezaji na ukuzaji wa uchumi kwa kupitia matumizi bora ya rasilimali zote muhimu za bahari.

Rais Dkt.Hussein Ali Mwinyi tayari amejipambanua yeye na Serikali yake kuwa dhamira yake ni kuijenga Zanzibar mpya kwa kupitia uchumi wa kisasa, Uchumi wa Buluuu (Blue Economy).

Katika moja ya hotuba zake, Dkt. Mwinyi alisema kuwa Uchumi wa Buluu ama uchumi wa bahari unafungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki, ujenzi wa viwanda vya samaki, ukulima wa mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi, matumizi bora ya rasilimali mbali mbali za bahari pamoja na shughuli za utalii wa fukwe na michezo ya baharini. Aliongeza kuwa uchumi wa Buluu haukamiliki bila ya kuwepo kwa Bandari za kisasa zenye ufanisi wa hali ya juu hivyo lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kujenga bandari kubwa za kisasa ambazo zitatoa huduma kwa wavuvi na kuchangia kukuza uchumi wa Zanzibar Mpya.









**KWA HATUA ILIYOFIKIWA SASA NI WAZI HAKUNA ASIEJUA KUWA UCHUMI WA BULUU UNAFAIDA KUBWA SANA KATIKA UKUZAJI WA UCHUMI WA NCHI YOYOTE ILE**




# DHANA YA UCHUMI WA BULUU

DHANA NZIMA YA UCHUMI WA BULUU NI PANA AMBAYO IMEBEBA SHUGHULI ZOTE ZA MSINGI ZINAZOFANYWA KATIKA BAHARI, MIONGONI MWAKE NI:-

- UVUVI WA AINA MBALIMBALI UKIWEMO WA KIBIASHARA NA USIO WA KIBIASHARA
- SHUGHULI ZA USAFIRISHAJI BAHARINI.
- SHUGHULI ZA UCHIMBAJI WA MADINI NA MAFUTA BAHARINI.
- SHUGHULI ZOTE ZA STAREHE NA MICHEZO KANDO YA BAHARI.
- UJEZI WA MELI NA VIWANDA VYA KUSINDIKA SAMAKI





MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BAHARI KUU IMEJIDHATITI KWA KIASI KIKUBWA KUENDELEZA KWA VITENDO SERA YA SERIKALI YA AWAMU YA NANE YA KUKUZA UCHUMI KUPITIA BAHARI.




### FAIDA

Kwa hatua iliyofikiwa sasa ni wazi hakuna asiejua kuwa uchumi wa Buluu unafaida kubwa sana katika ukuzaji wa uchumi wa nchi yoyote ile ambapo huongeza pato la taifa na pato la mwananchi mmoja mmoja endapo sekta hii itaangaliwa kwa jicho la kipekee kabisa. Jarida la TZ&BEYOND litazungumzia juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Mamlaka zake.

### MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BAHARI KUU (DSFA)

Kaimu Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu, Dkt. Emmanuel Sweke alisema taasisi hiyo imejidhatiti kwa kiasi kikubwa kuendeleza kwa vitendo Sera ya Serikali ya awamu ya nane ya kukuza Uchumi kupitia Bahari.

Sweke alisema tayari mamlaka kupitia Serikali kuu imefanya mapitio na kurekebisha baadhii ya sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinazotoa fursa kwa wadau kujitokeza katika kuwekeza kupitia bahari kuu ambayo ndio msingi mkuu wa uchumi wa Buluu.

“Sisi kama Mamlaka tayari tumeweka sheria, kanuni na taratibu nzuri ambazo zinawawezesha wadau kuja kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu ukizingatia kuwa moja ya nyenzo ya uchumi wa buluu ni uvuvi wa Bahari Kuu.”

Ili kukuza uchumi wa buluu inatakiwa kuwekwe mazingira rafiki kwa wavuvi wadogo wadogo wa ndani pamoja na wawekezaji wa ndani katika sekta nzima ya uvuvi.

“Katika kuwavutia wawekezaji wa ndani na hata wawekezaji wa nje, tumeweka motisha mbalimbali kama vile kuwapunguzia bei za leseni kwa wawekezaji wazawa pamoja na muda wa leseni ambapo wawekezaji wazawa wataweza kukata leseni kuanzia miezi mitatu na kuendelea, huku mwekezaji mgeni anatakiwa kukata kuanzia miezi sita na miezi 12.”



Wazawa wamewekewa fursa ambayo wanaweza kuingia ubia na watu wengine wenye uwezo katika kuwekeza katika uvuvi wa bahari Kuu na kuvua samaki na kunufaisha taifa kwa ujumla.

"Hii yote inatokana na kusudio la kuendana na sera ya Serikali ya kukuza uchumi wa Buluu unapowainua wavuvi wadogo wadogo na kuweka mazingira kwa wawekezaji kuja kuvua katika bahari kuu unakuza uchumi na kipato kupitia bahari ambayo imetuzunguka."

Aidha Dkt. Sweke alieleza kuwa tayari Mamlaka imeshafanya utafiti maalumu wa kutambua maeneo mbalimbali ya ukanda wa bahari yenye samaki wa kutosha kwa lengo la kuwaondoa usumbufu na gharama kwa wavuvi.

"Kupitia wadau tumefanya utafiti wa kujua maeneo hasa yenye samaki wa kutosha ambapo tunawaelekeza wavuvi sehemu za kwenda kuvua, hii inasaidia kuwaondolea usumbufu pamoja na gharama kubwa ambayo wangeweza kuitumia katika kutafuta samaki,"alieleza.

### WIZARA YA UCHUMI WA BULUU

Aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Uchumi wa Buluu, Abdallah Hussein Kombo alieleza kuwa wizara yake imeandaa mikakati mahsusi ya kukabiliana na changamoto yoyote ile itakayojitokeza wakati serikali ikitekelza sera yake ya kukuza uchumi kupitia Uchumi wa Buluu.

**DHANA YA UCHUMI WA BULUU NI MTAMBUKA NA INAHITAJI USHIRIKI WA KILA MMOJA WETU, NINAWAOMBA TUENDELEE KUIMARISHA MASHIRIKIANO BAINA YA SERIKALI NA SEKTA BINAFSI SAMBAMBA NA WADAU WENGINE WA MAENDELO.**



Aliongeza wizara imeanza na mkakati wa kukabiliana na changamoto ya uchache wa wataalamu wa kuzihudumia sekta zilizomo katika wizara hiyo ya uchumi wa Buluu.

"Tatizo hilo linazikabili nchi nyingi zinazopatikana na bahari, hivyo kuna haja ya kuwekwa mikakati itakayoimarisha uchumi kupitia sekta mbali mbali ikiwemo ya uvuvi ambao ndio shughuli mama katika uchumi wa Buluu."

Alibainisha kuwa, ili kufikia azma ya Zanzibar kunufaika na uchumi wa buluu, lazima sekta hiyo isimamiwe vyema na kuwekewa mkazo katika vipaumbele vya serikali ya Awamu ya Nane.

"Dhana ya uchumi wa buluu ni mtambuka na inahitaji ushiriki wa kila mmoja wetu, ninawaomba tuendelee kuimarisha mashirikiano baina ya serikali na sekta binafsi sambamba na wadau wengine wa maendelo."

Waziri Kombo alieleza kwamba iwapo changamoto zote zitafanyiwa kazi kimkakati, uchumi wa buluu utakuwa na tija kwa Zanzibar na watu wake na kuelekeza mbinu za utekelezaji ikiwemo ya kuzifanyia mapitio sera na sheria zilizopitwa na wakati sambamba na kuwekwa mpango mzuri wa matumizi ya bahari (Special planning).










**ZANZIBAR INA RASILIMALI KUBWA YA WAVUVI WADOGO WADOGO WENYE UJUZI LAKINI WANAKOSA MBINU NA VIFAA VYA KISASA**

WAKATI UMEFIKA SASA WAZANZIBARI NA WAATANZANIA KWA UJUMLA KUANZA KUVUA KATIKA BAHARI KUU

"Hatuwezi kuwa na uchumi wa buluu tukaitumia bahari kama shamba la bibi, lazima tuwe na mpango madhubuti utakaoonyesha namna gani tutakuwa na nia ya kuitumia bahari yetu."

### TUME YA MIPANGO

Afisa wa Tume ya Mipango, Saleh Saad Mohammed alibainisha kuwa, iwapo Serikali itajidhatiti katika kutekeleza kwa vitendo dhana nzima ya Uchumi wa Buluu, kuna fursa nyingi zitaibuliwa na kuimarisha uchumi wa Zanzibar na watu wake.

"Miongoni mwa fursa hizo ni pamoja na ujenzi wa bandari ya uvuvi baina ya serikali na sekta binafsi, ujenzi wa sehemu ya kuhifadhia samaki na kujenga kiwanda cha uzalishaji barafu itakayotumika kuhifadhia samaki na mazao mengine ya baharini." Wakati umefika sasa Wazanzibari na watanzania kwa ujumla kuanza kuvua katika bahari kuu ili kujiongezea tija na faida.

"Zanzibar ina rasilimali kubwa ya wavuvi wadogo wadogo wenye ujuzi lakini wanakosa mbinu na uwezo wa kufika katika maji makubwa hivyo watakapowezeshwa pamoja na kujengewa uwezo, watavua katika bahari kuu na kuongeza kipato chao."

### WAVUVI

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wavuvi Kojani,Omar Mohamed Ali alibainisha kuwa kwa sasa Wazanzibari wategemee bahari kuwa kimbilio lao salama, na wanapaswa kuipongeza Serikali ya awamu ya nane kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha uchumi wa nchi unatokana na bahari.

# MABADILIKO
# Tabia nchi

**Sote tunapaswa kuwajibika kutunza mazingira kwa minajili ya vizazi vya leo na vya kesho**




"Nampongeza Rais wetu Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuonesha juhudi za kuboresha sekta ya uvuvi kutokana na ukweli kwamba jiografia ya Zanzibar imezungukwa na bahari na wananchi wake wanategemea sana sekta nzima ya Uvuvi.

Aidha Khamis Mussa Makame Mvuvi kutoka Bububu yeye alisema serikali imejidhatiti kuongeza thamani ya shughuli za uvuvi na matumizi ya bahari hivyo anaona kuwa ajira nyingi kwa vijana zitazalishwa.

"Hapo nyuma ukiwa mvuvi ni kazi ya kudharaulika ila sasa uvuvi unaonekana ni nyenzo nzima ya kukuza na kuboresha uchumi wa nchi na kipato cha mtu mmoja mmoja."

Hata hivyo anaeleza kuwa ni wakati wa Serikali kushirikiana na wananchi bega kwa bega katika kuhakikisha sera yake ya uchumi wa Buluu inakuwa ipasavyo na kuwanufaisha wananchi wake.

### WANASIASA

Katibu wa Chama cha Demokrasia Makini, Ameir Hassan Ameir alisema kuwa Serikali kupitia wadau wake mbalimbali inapaswa kujipambanua kwa kina juu ya sera ya uchumi wa Buluu ambapo anaamini kuna nafasi kubwa na nzuri ya kuifanya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kuwa na uchumi uliobora kupitia bahari.

" Kwa mfano hapa kwetu Zanzibar, Sekta nzima ya uvuvi huchangia asilimia 2.6 ya pato ghafi la Zanzibar ambapo hutoa ajira za moja kwa moja zaidi ya 200,000 ndani ya visiwa hivi huku zaidi ya watu 400,000 wakiwa wanategemea sekta hii."

Aliongeza kuwa,Kuimarika kwa sekta nzima ya uvuvi na bahari huchangia kukuwa kwa uchumi wa nchi pamoja na wananchi kwa ujumla hivyo serikali inapaswa kuendelea kuweka mipango iliyothabiti katika kutekeleza sera yake ya kukuza uchumi kupitia Bahari (Blue Economy).



*KWA MFANO HAPA KWETU ZANZIBAR, SEKTA NZIMA YA UVUVI HUCHANGIA ASILIMIA 2.6 YA PATO GHAFI LA ZANZIBAR AMBAPO HUTOA AJIRA ZA MOJA KWA MOJA ZAIDI YA 200,000 NDANI YA VISIWA HIVI HUKU ZAIDI YA WATU 400,000 WAKIWA WANATEGEMEA SEKTA HII*



# UCHUMI WA BULUU NURU YA ZANZIBAR





Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Chama cha UPDP Hamad Ibrahimu alieleza kuwa ili kukuwa mapema kupitia uchumi wa Buluu Serikali inapaswa kudhibiti uvuvi haramu pamoja na kuwainua wanawake kwa kuwapatia nyenzo mbalimbali zitakazo wawezesha kumudu shughuli zao za baharini. “Asilimia mbili ya wanawake duniani kote hujishughulisha na shughuli mbalimbali za bahari hivyo serikali ikiweka mazingira mazuri kwa wanawake hawa katika kujiendeleza na shughuli zao huchangia kukua na kukuza sekta ya bahari pamoja na kudhibiti uvuvi haramu.”

Ili kuwa na uchumi endelevu na kwenda sambamba na mataifa mengine Serikali inapaswa kuwa na mipango imara inayotekeleza katika uchumi wa Buluu ambao ndio kiini cha uchumi wa kileo.

## NINI KIFANYIKE

Ili kufanikisha nia njema hii ni vizuri kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuiona dhana ya uchumi wa buluu kama fursa kwa ajili ya fikra na mabadiliko ya kiuchumi, zipo nchi mbalimbali zilizojikita katika uchumi wa buluu kama jukwaa la kujikomboa na kujiendeleza kiuchumi.



ILI KUKUWA MAPEMA KUPITIA UCHUMI WA BULUU SERIKALI INAPASWA KUDHIBITI UVUVI HARAMU PAMOJA NA KUWAINUA WANAWAKE KWA KUWAPATIA NYENZO MBALIMBALI ZITAKAZO WAWEZESHA KUMUDU SHUGHULI ZAO ZA BAHARINI.




# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

## MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA (TMDA)

TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

## KUHUSU TMDA

*Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ambayo ilikuwa ikijulikana kama Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambayo ina jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, bidhaa za tumbaku, chanjo, vifaa tiba na vitendanishi.*

*Iliyokuwa TFDA ilibadilishwa jina na kuwa TMDA mnamo tarehe 1 Julai, 2019 kufuatia marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 kupitia Sheria ya Fedha, Na. 8 ya mwaka 2019 ambayo mbali na kubadili jina la Sheria hiyo kuwa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219, pia ilihamisha majukumu ya kudhibiti ubora na usalama wa chakula na vipodozi kwenda katika Sheria ya Viwango, Sura 130.*

**DIRA** | Kuwa Mamlaka inayoongoza katika kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, chanjo, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine zinazohusiana na afya kwa wote

**DHIMA** | Kulinda afya ya jamii kwa kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, chanjo, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine zinazohusiana na afya.

### MAJUKUMU

1. Kusajili na kutoa vibali vya majengo ya kutengeneza na kuuza dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
2. Kukagua maeneo ya kutengeneza na kuuza dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
3. Kukagua shehena za bidhaa za dawa, chanjo tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya forodha na kwenye maghala ya kuhifadhia bidhaa hizi
4. Kutoa vibali vya kuingizia na kusafirisha nje ya nchi bidhaa za dawa, chanjo, tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
5. Kusajili bidhaa za dawa, chanjo, tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi kabla ya kuruhusiwa kuuzwa katika soko la Tanzania
6. Kudhibiti majaribio ya dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku na vifaa tiba na kufuatilia madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa hizi
7. Kudhibiti matangazo ya dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi
8. Kutoa elimu kwa umma

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),**
**S.L.P 77150, Dar es Salaam au**
**S.L.P 1253 Dodoma**
**Simu: +255 222 450512/450751/452108**
**Simu ya Bure: 0800110084**
**Nukushi: +255 222 450793**
**Barua Pepe: info@tmda.go.tz Tovuti: www.tmda.go.tz**

0800110084 @tmda_tanzania @tmda tanzania www.tmda.go.tz "TMDA Hulinda Afya ya Jamii"



ASILIMIA MBILI YA WANAWAKE DUNIANI KOTE HUJISHUGHULISHA NA SHUGHULI MBALIMBALI ZA BAHARI HIVYO SERIKALI IKIWEKA MAZINGIRA MAZURI KWA WANAWAKE HAWA KATIKA KUJIENDELEZA NA SHUGHULI ZAO HUCHANGIA KUKUA NA KUKUZA SEKTA YA BAHARI PAMOJA NA KUDHIBITI UVUVI HARAMU






MIPANGO YA MAENDELEO YA KITAIFA YA MUDA MREFU (VISION 2050), IMEWEKA UMUHIMU WA KUONGEZA VIPATO










TIB
DEVELOPMENT
BANK
Your Partner for Growth
Chagua Benki ya Maendeleo TIB
Mshirika Wako Katika Maendeleo
Benki inatoa mikopo kwenye:
• Uendelezaji wa miundombinu
• Maendeleo ya Viwanda
• Uchimbaji wa madini
• Mafuta na Gesi
• Huduma
md@tib.co.tz
www.tib.co.tz

# UCHUMI WA BULUU *kisima cha ajira*



## UCHUMI WA BULUU KISIMA CHA
# AJIRA

MOJA ya changamoto zinazoikabili duniani kwa muda mrefu ni tatizo la ajira hasa kwa vijana waliosoma na wasiosoma. Ubaya wa tatizo hili ambalo linaisumbua dunia, lakini hakuna mfanano wala mlinganyo wa namna yeyote ya utatuzi wake, kila nchi inasimama kivyake katika njia na namna za kutafuta suluhu.

Katika heka heka hizo za kutafuta suluhu ndipo ilipoibuka dhana ya uchumiwa wa buluu (Blue Economy) ambayo sasa imeanza kushika kasi katika baadhi ya nchi za ukanda wa Afrika Mashariki hasa Tanzania na Zanzibar ikiwa kinara.

### MWASISI WA DHANA YA UCHUMI WA BULUU

Kimsingi dhana ya uchumi blue ambayo kwa Zanzibar inatambulika kama uchumi wa Buluu, iliasisiwa na Profesa Gunter Pauli mwaka 1994 kupitia kitabu chake alichokipa jina la "The Blue Economy: 10 years – 100 innovations – 100 million jobs".

Prof. Pauli alilinganisha uchumi wa buluu na uchumi wa kijani, kwa kusema shughuli za uchumi wa buluu zina faida zaidi na kuongeza mzunguko wa fedha na matokeo yake ni ya muda mfupi.

Na hili linawezekana kwa mataifa mengi yanayopakana na bahari yanatumia uchumi wa buluu kama njia moja ya kukuza maendeleo ya wananchi wao.

Hata hivyo mafanikio ya utekelezaji wa uchumi wa buluu yanategemea ni vipi nchi husika inatumia na kuhifadhi maeneo yake ya bahari pamoja na rasilimali zake kwa njia endelevu.

Tafiti zinaeleza kuwa sekta zinazohusiana na uchumi wa bahari zinafursa kubwa kuliko sekta nyengine katika ukuaji wa uchumi na upatikanaji wa ajira kwa watu wa rika na kada mbalimbali.

### UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR

Kwa upande wa Zanzibar mipango ya maendeleo ya kitaifa ya muda mrefu (Vision 2050), imeweka umuhimu wa kuongeza vipato vya wananchi na kukuza uchumi na kuwa na maendeleo endelevu kupitia uchumi wa buluu.







# fursa za bahari





Hivyo, uwekezaji katika uchumi wa buluu una mazingatio maalum katika kuleta maendeleo ya bahari na rasilimali zake.

Kwa sababu Zanzibar ni nchi ya visiwa, uchumi wa bluu unatarajiwa kuleta faida kubwa kwa kutumia rasilimali za bahari na fukwe kwa njia endelevu ili kukuza uchumi wa nchi, ustawi wa watu, upatikanaji wa ajira na uhifadhi wa mazingira ya bahari.

**FURSA ZA BAHARI**

Bahari ina fursa kubwa na rasilimali zake ni nyingi miongoni mwake zikiwa ni chanzo cha nishati, chakula, usafiri wa baharini na kivutio cha utalii vyote hivi ni vichocheo vikubwa kwa ustawi wa maisha ya wananchi na ukuaji wa uchumi. Pamoja na ukweli huo bado rasilimali zinazotokana na bahari zinakabiliwa na changamoto kadhaa kama vile ongezeko la idadi ya watu, mabadiliko ya tabia nchi, matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali hizo, kuwepo kwa maharamia na harakati za maendeleo kama vile ujenzi ambazo kwa kiasi zinatishia usalama wa kutoweka kwa rasilimali za bahari.

Wachambuzi wa mambo wanaweka wazi kuwa uchumi unaotokana na rasilimali za bahari, unatarajiwa kutatua changamoto hizo na kuwa ni fursa na nafasi kubwa zaidi kwa ukuaji wa uchumi endelevu wa Zanzibar ambao utaendana na mazingira halisi ya wananchi wa Zanzibar.

Kupitia uchumi wa buluu Zanzibar ina fursa za kuongeza ajira, kukuza usalama wa chakula, kulinda na kusimamia mazingira ya bahari kwa maisha ya sasa na ya baadae. Kama tunavyojua Zanzibar ipo eneo zuri kijiografia na eneo lake la bahari ni kubwa kuliko ardhi yake ambapo kwa zaidi ya miongo miwili Zanzibar imekuwa ikitegemea ndogo ya utalii katika kukuza uchumi.

Sekta ya utalii inawezwa kuimarishwa na kuvutia wawekezaji wengi wa vipato vya juu kwa kuongeza vivutio vya utalii. Miongoni mwa vivutio vya utalii ni pamoja na fukwe, michezo ya baharini, uzamiaji, uvuvi wa michezo, urukaji kwa vishada na uwepo wa maegesho ya boti. Kuna fursa nyingi za uchumi wa buluu ambazo zinahitaji nguvu ya pamoja kuziendeleza, ili kufanikisha hili ipo haja ya kuiunga mkono serikali ili kufanikisha dhamira hiyo njema na kumnufaisha kila mwananchi.





# HOTELI

ZANZIBAR

SEKTA YA UTALII INAWEZA KUIMARISHWA NA KUVUTIA WAWEKEZAJI WENGI WA VIPATO VYA JUU KWA KUONGEZA VIVUTIO VYA UTALII.

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# MIFUMO YA HUDUMA BINAFSI KWA **MWANACHAMA NA MWAJIRI**

Mifumo hii ni ya mwajiri **"Employer Portal"** na mwanachama **"Member Portal"** inapatikana kupitia tovuti ya Mfuko **"www.nssf.or.tz"** bofya kifute cha **"Self Service"** (Huduma Binafsi).




- Mfumo wa **"Employer Portal"** ni maalum unaowawezesha waajiri kuangalia michango ya wafanyakazi wao, unaohamasisha uwazi na uwajibikaji kati ya Mfuko na mwajiri.
- Mfumo wa **"Member Portal"** unamuwezesha mwanachama kupata taarifa za michango yake.

@NssfTanzania






# FURSA

## UCHUMI WA BULUU

MIONGONI MWA VIVUTIO VYA UTALII NI PAMOJA NA FUKWE, MICHEZO YA BAHARINI, UZAMIAJI, UVUVI WA MICHEZO, URUKAJI KWA VISHADA NA UWEPO WA MAEGESHO YA BOTI.



# RAIS MWINYI

## *Kiongozi* MBEBA MAONO

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, sasa anatazamwa kama mbeba maono wa maendeleo endelevu ya Zanzibar na pengine Tanzania kwa ujumla.

Dhana hiyo inabebwa na mwenendo wake wa kiutendaji tangu alipoingia madarakani mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 25, 2020.

Rais Dkt. Mwinyi amekuwa kinara wa harakati za maendeleo na katika kudhihirisha hilo ameamua kuitumia Bahari kuwa kimbilio la wengi kwa kuja na dhana ya uchumi wa buluu.

Uchumi wa Buluu (Blue Economy) ni uchumi unaohusisha shughuli zote za ndani na nje ya eneo la bahari kwa maana ya fukwe na maji yenyewe.

Uamuzi wake huu ndio unaomfanya kiongozi huyu mwenye kutenda zaidi ya kusema kutazamwa kama Rais mbeba maono ambaye pamoja na kutekeleza, kuheshimu na kuthamini yaliyofanywa na watangulizi wake, lakini pia amekuja na yake yanayoonekana kubeba maana halisi ya kumkomboa mwananchi.

Katika kufanikisha hilo ameahidi kuijenga



Zanzibar mpya kwa kupitia uchumi wa Buluu.

Alitoa ahadi hiyo katika hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi lililofanyika katika ukumbi wa Baraza hilo Chukwani, nje kidogo ya Jiji la Zanzibar.

Ahadi hiyo ilitolewa mbele ya viongozi waliopo madarakani na wastaafu akiwemo Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Zanzibar Amani Abeid Karume, Dk. Ali Mohammed Shein, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, Maryam Mwinyi, wake wa Marais wastaafu, mabalozi na viongozi mbalimbali.

Katika hotuba yake hiyo, Rais Mwinyi alisema kuwa moja ya ahadi yake kubwa aliyoitoa kwa wananchi na ambayo imeelezwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni kujenga uchumi wa kisasa wa Buluu (Blue Economy).

Uchumi wa Buluu ama uchumi wa bahari unafungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki, ujenzi wa viwanda vya samaki, ukulima wa mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi, matumizi bora ya rasilimali mbali mbali za bahari pamoja na shughuli za utalii wa fukwe na michezo ya baharini.

UCHUMI WA BULUU (BLUE ECONOMY) NI UCHUMI UNAOHUSISHA SHUGHULI ZOTE ZA NDANI NA NJE YA ENEO LA BAHARI KWA MAANA YA FUKWE NA MAJI YENYEWE.






# TZ&BEYOND




***Jarida hili linalowafikia watu wa rika na kada*** mbalimbali ndani na nje ya Tanzania limelenga kukupa maarifa ambayo huwezi kuyapata kwenye jarida lolote **Tanzania**.

**TZ&BEYOND** limejikita kwenye kuchambua masuala ya siasa, Bunge, Uchumi, Mazingira, Uhifadhi na Habari za kimataifa dhamira yake kuu ni kuwa darasa mikononi mwako.

***TUNA MWANZO, HATUNA MWISHO***

**USIKOSE KUSOMA MAJARIDA YETU KUPITIA TOVUTI**

www.tz&beyond.co.tz



**BANDARI MPYA**

**SERIKALI YA AWAMU YA NANE INA MALENGO YA KUJENGA BANDARI KUBWA YA KISASA KATIKA MAENEO YA MANGAPWANI ITAKAYOKUWA NA SEHEMU KADHAA ZA KUTOLEA HUDUMA ZIKIWEMO SEHEMU ZA KUHUDUMIA MELI ZITAKAZOBEBA MAFUTA NA GESI, CHELEZO KWA AJILI YA MATENGENEZO YA MELI, ENEO LA KUHUDUMIA MELI**

**SERIKALI YA AWAMU YA NANE ITASIMAMIA KWA UMAKINI NIDHAMU NA UWAJIBIKAJI WA WATUMISHI WA UMMA NA HAITAKUWA NA MUHALI KWA MTENDAJI YOYOTE AMBAE HATOWAJIBIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAKE.**



RAIS WA ZANZIBAR DK.HUSSEIN MWINYI AKIWA KATIKA PICHA YA PAMOJA NA BALOZI WA KUWAIT NCHINI TANZANIA MHE. MUBARAK MOHAMMED ALSEHAIJAN

Rais Dkt. Mwinyi alisema uchumi wa Buluu haukamiliki bila ya kuwepo kwa Bandari za kisasa zenye ufanisi wa hali ya juu.

### RUSHWA NA UFISADI

Rais Dkt. Mwinyi alieleza kuwa miongoni mwa mambo yanayodhoofisha misingi ya utawala bora ni rushwa, uzembe, kukosa uwajibikaji, kutofuata sheria na kukiukwa kwa maadili hivyo, alisisitiza kuwa Serikali ya Awamu ya Nane itakabiliana ipasavyo na vitendo vyote vinavyoathiri utekelezaji wa misingi ya utawala bora.

Alirejea ahadi yake kwa wananchi mbele ya Baraza hilo kwamba atapambana na rushwa na ufisadi bila kigugumizi wala kuoneana muhali na kuwaomba Wawakilishi na Wananchi wote wamuunge mkono wakati wa mapambano hayo.

"Tutashinda vita hii endapo wananchi pia watatuunga mkono. Sina shaka kuwa kwa vile wao, kwa wingi wao, wanachukia rushwa na ufisadi, watakuwa tayari kutoa ushirikiano wao katika mapambano haya. Ni matumaini yangu pia vyombo husika katika jambo hili vitatekeleza wajibu wao."

### MKONO WA POLE

Katika hotuba pia, alitumia fursa hiyo kutoa pole kwa Chama cha ACT Wazalendo, ndugu, jamaa na marafiki kufuatia kifo cha ndugu Abubakar Khamis Bakari ambaye aliwahi kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Katiba na Sheria katika Serikali ya Awamu ya Saba kipindi cha kwanza.

### HAKUNA MUHALI

Rais Mwinyi aliweka wazi kuwa kiongozi yoyote atakayemteua kwa mamlaka aliyonayo kikatiba, atamuwajibisha mara moja pindi tu akibaini na kujiridhisha kuwa anajihusisha na vitendo vya rushwa na ufisadi.

Uteuzi wa viongozi na watendaji katika Serikali yake utazingatia uwezo wa mtu kitaaluma, uwajibikaji na uaminifu.

Serikali ya Awamu ya Nane itasimamia kwa umakini nidhamu na uwajibikaji wa watumishi wa umma na haitakuwa na muhali kwa mtendaji yoyote ambae hatowajibika katika utekelezaji wa majukumu yake.

Aliongeza kuwa atakayeshindwa kuwajibika aelewe kuwa atawajibishwa kwani uzembe na ukosefu wa nidhamu kazini huzorotesha maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kwa hivyo, tabia hiyo hatoivumilia.

Aidha aliwataka viongozi wote waliopewa dhamana katika nafasi mbali mbali wawe wabunifu na waweze kuishauri Serikali juu ya masuala yanayohusu fani na utaalamu wao huku akisisiza kwamba Serikali haitowavumilia viongozi wenye kusubiri kuambiwa kutoka kwake au Serikalini nini wafanye katika kutekeleza majukumu yao.

### MAFUTA NA GESI

Akieleza kuhusu sekta ya mafuta na gesi, Rais Mwinyi alisema kwamba Serikali ya Awamu ya Nane itaziimarisha na kuzijengea uwezo wa kitaaluma na nguvukazi Kampuni ya Mafuta Zanzibar (ZPDC) na Mamlaka ya Usimamizi wa Mafuta na Gesi (ZPRA) ili ziweze kuiongoza sekta hiyo muhimu.

Vile vile, alisema kwamba Serikali itaendelea kushirikiana na Kampuni mbali mbali zenye dhamira njema ya kuwekeza hapa nchini katika sekta hiyo.

### BANDARI MPYA

Serikali ya Awamu ya Nane ina malengo ya kujenga bandari kubwa ya kisasa katika maeneo ya Mangapwani itakayokuwa na sehemu kadhaa za kutolea huduma zikiwemo sehemu za kuhudumia meli zitakazobeba mafuta na gesi, chelezo kwa ajili ya matengenezo ya meli, eneo la kuhudumia meli zinazobeba mizigo na makontena, bandari ya uvuvi pamoja na bandari ya meli za kitalii.



# GAS

**Akieleza kuhusu sekta ya mafuta na gesi, Rais Mwinyi alisema kwamba Serikali ya Awamu ya Nane itaziimarisha na kuzijengea uwezo wa kitaaluma na nguvukazi Kampuni ya Mafuta Zanzibar (ZPDC) na Mamlaka ya Usimamizi wa Mafuta na Gesi (ZPRA) ili ziweze kuiongoza sekta hiyo muhimu. Vile vile, alisema kwamba Serikali itaendelea kushirikiana na Kampuni mbali mbali zenye dhamira njema ya kuwekeza hapa nchini katika sekta hiyo.**



**DHAMIRA YA SERIKALI NI KUIMARISHA BANDARI ZA WETE NA SHUMBA MJINI NA KUENDELEA NA MATAYARISHO YA UJENZI WA BANDARI YA MAFUTA NA GESI HUKO MANGAPWANI**



Aligusia kuwepo kwa malalamiko ya wafanyabiashara kuhusu kucheleweshwa mizigo yao bandarini na msongamano wa makontena katika Bandari ya Malindi, vitendo vya rushwa na kukosa uwajibikaji kwa baadhi ya watumishi wa bandarini.

Alieleza dhamira ya Serikali ya kuimarisha bandari za Wete na Shumba Mjini na kuendelea na matayarisho ya ujenzi wa bandari ya mafuta na gesi huko Mangapwani na kuiimarisha bandari ya Mkoani ili iweze kuhudumia meli kubwa kutoka nje moja kwa moja kwa lengo la kunyanyua uchumi na biashara kwa kisiwa cha Pemba.

## KODI

Kwenye eneo la kodi, Serikali ya Awamu ya Nane itaongeza nguvu katika upanuzi wa wigo wa kodi na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha kwamba kila mtu anayestahili kulipa kodi analipa kodi stahiki. "Tutahakikisha kwamba kila senti inayoongezeka katika mapato ya Serikali inaelekezwa katika kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Tutaziba mianya ya upotevu wa fedha za Serikali ambayo inaipunguzia Serikali uwezo wake wa kuwahudumia wananchi",alisema Rais Mwinyi.

Aidha, alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Nane, itaweka mazingira mazuri ya uwekezaji na uendeshaji wa biashara ili sekta hizo ziwe na mchango mkubwa zaidi katika kukuza ajira na katika Pato la Taifa.


TIPER
TANZANIA INTERNATIONAL PETROLEUM RESERVES L.T.D




TIPER
BULK STORAGE





**TIPER** the joint venture company between the government of Tanzania and Oryx Energies SA (OESA) based in Geneva with equal shares 50% each operates the largest storage facility for petroleum in the country. Current storage capacity is 253.7 million litres.

TIPER which used to be known as Tanzanian Italian Petroleum Refining (TIPER) Company Limited, commissioned refinery business in 1966. In year 2000, the refinery business ceased. In 1999 Agippetrol International (BV) - "Agip" sold its assets in TIPER as well as the 50% shareholding of the company to Oryx Energies SA., GENEVA (OESA). The remaining 50% shares continued to be owned by the Government of Tanzania.

Following the liberalization of the downstream petroleum subsector in Tanzania, TIPER found it uneconomical to operate as a refinery. In mid-2000, the company changed its main objective from refining to petroleum product storage. The refinery was decommissioned, scrapped and the plant was then converted in to a refined petroleum storage terminal, whose core business is the bulk storage and handling of refined petroleum products with delivery of the customer's product through cross pumping to other terminals, back-loading for onward transshipment and truck loading for onward sale at local commercial and retail outlets as well as for transit.






**TIPER** operating as a bulk liquid storage entity, stores low sulphur diesel (AGO), Premium Motor Spirit " (PMS), Dual Purpose Kerosene (DPK) and Heavy Fuel Oil (HFO 180) which is widely used in industrial applications. TIPER operating as storage facility has facilitated to a greater extent the availability of petroleum products in the country as well as for neighboring land locked countries.

## TIPER'S CURRENT STORAGE CAPACITY BY PRODUCT IS SHOWN BELOW:

| Product | Capacity (Litres) |
|---|---|
| Diesel (AGO) | 180,246,000 |
| Premium Motor Spirit " (PMS) | 56,302,000 |
| Dual Purpose Kerosene (DPK) | 5,723,000 |
| HFO 180 | 11,383,000 |
| Total Storage Capacity | 253,654,000 |



# TIPER's future plan include:

- To increase the capacity by adding more tankage to facilitate the envisaged opera tions of a special bonded warehouse and eventual Strategic Petroleum Reserve (SPR).
- Lifting the operating standards in all fronts especially the HSSEQ and attain the ISO certification.
- To gain validation in practical terms, to become the hub for petroleum supply chain for East and Southern Africa.
- Enhancing Truck Loading Operations to facilitate operational efficiency for Various customers.







SERIKALI ITAWEKA MAZINGIRA MAZURI YA UWEKEZAJI NA UENDESHAJI WA BIASHARA ILI ZIWE NA MCHANGO MKUBWA KATIKA KUKUZA AJIRA NA PATO LA TAIFA.

# Ulaya

## NA UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi ameupongeza utayari wa Umoja wa Ulaya (EU) wa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar ikiwa ni pamoja na kuanzisha programu mbali mbali za maendeleo.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu Jijini Zanzibar wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU), nchini Tanzania Manfredo Fanti akiwa amefuatana na ujumbe wake.

Katika maelezo yake Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa hatua ya Umoja wa Ulaya (EU) ya kuisaidia Zanzibar katika kuimarisha programu mbali mbali za maendeleo zitasaidia kwa kiasi kikubwa katika kutekeleza Sera yake ya Uchumi wa Buluu. Rais Dk. Mwinyi alieleza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshaweka mikakati madhubuti katika kuhakikisha Sera yake ya Uchumi wa Buluu inatekelezeka ipasavyo, hivyo, hatua za Umoja wa Ulaya (EU) kuziunga mkono juhudi hizo zitaleta mafanikio makubwa.

Aliongeza kuwa juhudi za makusudi zimekuwa zikichukuliwa katika kuhakikisha utunzaji wa mazingira unapewa kipaumbele hasa uhifadhi wa mazingira ya bahari hatua ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuyahifadhi na kuyalinda mazalio ya viumbe vya baharini.

Aidha, Rais Dk Mwinyi alieleza mikakati iliyowekwa na Serikali katika kuwasaidia wakulima wa zao la mwani ambao asilimia kubwa ni wanawake ikiwa ni pamoja na kuanzisha utaratibu wa kulisarifu zao hilo hapa hapa nchini badala ya kuliuza kama malighafi.

Alisema kuwa tayari kiwanda cha mwani kinajengwa huko Chamanangwe kisiwani Pemba, ikiwa ni miongoni mwa juhudi za kuhakikisha zao hilo linawanufaisha wakulima wake kwa kiasi kikubwa sambamba na kulipatia soko la uhakika litakalowaongezea kipato wakulima wa zao hilo.

Pia, Rais Dk. Mwinyi alieleza mikakati iliyowekwa na Serikali katika kuuimarisha Uchumi wa Buluu ikiwa ni pamoja na kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo katika kuhakikisha wanapata uwezo wa kuvua kisasa na kuweza kupata pato kutokana na kutumia vifaa na nyenzo za kisasa sanjari na kuwasaidia wafugaji wa samaki.



# Utalii
## ZANZIBAR









Rais Dk. Mwinyi pia, alizungumzia suala zima la kuimarisha Mji Mkongwe wa Zanzibar ambapo hivi sasa hatua za makusudi zimekuwa zikichukuliwa katika kuhakikisha Mji huo unaleta haiba yake ya asili huku akiupongeza Umoja huo kwa kuunga mkono harakati za utalii katika Mji Mkongwe hasa katika Matamasha likiwemo Tamasha la Sauti za Busara.

Sambamba na hayo, Rais Dk. Mwinyi alimueleza kiongozi huyo mikakati iliyowekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutafuta vyanzo vyengine vya nishati ya umeme hapa Zanzibar na kuipongeza EU kwa kuunga mkono suala hilo.

Rais Dk. Mwinyi pia, alitumia fursa hiyo kuzikaribisha nchi za Umoja wa Ulaya kuja kuwekeza Zanzibar kwani bado kuna fursa mbalimbali hasa katika sekta ya uwekezaji na utalii kwa azma ile ile ya kuunga mkono Sera ya Uchumi wa Buluu.

Mapema Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU), nchini Tanzania Manfredo Fanti alimueleza Rais Dk. Mwinyi mipango na mikakati madhubuti iliyowekwa na Umoja huo katika kuisaidia Zanzibar kuimarisha na kuendeleza programu mbali mbali za maendeleo.

Katika mazungumzo hayo, Balozi Fanti alipongeza juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Dk. Mwinyi na kueleza matumaini makubwa ya umoja huo ya kuiona Zanzibar inafunguka kimaendeleo. Alieleza hatua zilizofikiwa na Umoja huo za kuanzisha programu za maendeleo katika visiwa vya Unguja na Pemba kwa mwaka huu na kuendelea kwa mwaka ujao.

Akieleza miongoni mwa programu hizo ni pamoja na kuhakikisha suala zima la mazingira linapewa kipaumbele hasa ikizingatiwa kuwa Umoja huo umetenga bajeti maalum ya programu hizo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Zanzibar. Alieleza kuwa hatua hiyo itasaidia hata kuwaendeleza wavuvi, kutunza misitu na uhifadhi wa mazingira yote ya baharini pamoja na viumbe vyake sambamba na kuendeleza hatua za kukabiliana na Tabianchi. Pamoja na hayo, Balozi huyo alieleza azma ya Umoja huo kuunga mkono suala la jinsia kwa kuwasaidia wanawake katika kujiendeleza kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Sambamba na hayo, Balozi Fanti alimuhakikishia Rais Dk. Mwinyi kwamba Umoja wa Ulaya (EU), utahakikisha unaiunga mkono Zanzibar katika nyanja zote za Uchumi wa Buluu ambao ndio Dira ya uchumi wa Zanzibar.









# UCHUMI WA BULUU

## NENO LISOKWISHA HAMU

Bahari zenye afya na mazingira ya baharini ni muhimu kwa uchumi wetu na uhai wa muda mrefu wa dunia. Ni mapafu ya ulimwengu wetu, ikitoa nusu ya oksijeni tunayopumua. Wanahesabu 16% ya protini ya wanyama tunayoingiza na kutumika kama msingi wa shughuli anuwai za kiuchumi ambazo zinakuza maendeleo na ajira. Wao ni chanzo kizuri cha lishe.

Maji yetu na bahari zina jukumu muhimu katika maisha yetu. Tunawategemea chakula na utalii, usafirishaji, na nishati ya kijani kibichi. Wao ni chanzo tajiri cha viumbe hai na hutoa huduma muhimu kwa mifumo ya mazingira.

Walakini, mara nyingi wanakabiliwa na vitisho anuwai tofauti, kutoka kwa samaki wenye kuchosha hadi vizuizi kuongezeka kwa mazingira.

FSF-IHCE imejitolea kukuza ukuaji wa muda mrefu katika sekta za baharini na usafirishaji kupitia mafunzo ya uchumi wa bluu na elimu. Kama tuko katikati ya shida kubwa inayosababishwa na janga la coronavirus. Haja ya kukumbuka na kuelewa umuhimu wa bahari, iwe ya kitamaduni, kijamii, au kiuchumi, haijawahi kuwa ngumu zaidi.Lengo la FSF-IHCE ni kuhakikisha kuwa sayansi, ubunifu, na elimu inachangia mabadiliko ya Uchumi Endelevu wa Buluu. Kwa kuzingatia pwani zilizolindwa, bahari, ukanda wa pwani, na maji ya ndani.

Elimu na mafunzo katika Uchumi Bluu inapaswa kuratibiwa vizuri ili kukuza ukuaji wa sekta ya bahari, na Uchumi wa Bluu kwa hivyo unaweza kutoa moja ya fursa kubwa zaidi kwa mafanikio ya biashara.

Kupitia mpango wa FSF-IHCE wa mafunzo ya mafunzo katika uchumi wa bluu, hii itasababisha kupelekwa kwa suluhisho za kupunguza taka za majini, kama vile plastiki, kupunguza mabadiliko ya hali ya hewa baharini, matumizi salama na usimamizi wa nishati ya bahari, maendeleo ya bidhaa mbadala , kama vile uingizwaji wa plastiki unaoweza kuoza, chakula kipya na mifumo ya chakula, upangaji mkakati wa pwani na bahari, na usimamizi wa bahari. Wanadamu, maisha ya ikolojia, na maisha ya bioanuwai yote yanategemea hatua ya ujasiri na ya pamoja.

FSF-IHCE imejitolea kuweka ajenda ya kijamii mahali ambayo inapeana kipaumbele kwa watu na uchumi wa bluu katika ushirikiano na mipango ya muda mrefu. Tunahitaji msaada wako kwa njia ya ushirikiano na michango kutusaidia kutimiza malengo yetu. Na kampeni za maendeleo endelevu ya bluu katika maeneo yote ya ulimwengu.

# WASOMI WAUCHAMBUA UCHUMI WA BULUU



PROF. LIPUMBA ALIFAFANUA KUWA NCHI ZA VISIWA VIDOGO ZINAZOENDELEA ZINADHIBITI ASILIMIA 30 YA BAHARI NA BAHARI ZOTE.

DHANA ya uchumi wa Buluu (Uchumi wa Buluu) ilikuwepo kwa nchi nyingi zilizozungukwa na bahari.

Hata hivyo kwa Tanzania hasa visiwani dhana hii imeanza kushika kasi baada ya kupewa mashiko na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi.

**NINAONA WAWEKEZAJI WANAKUJA NA NINAAMINI NI MUHIMU SANA KWAMBA, KIMATAIFA, TUENDELEE KUZINGATIA, ILI TUWEZE KUJENGA USHIRIKIANO KATI YA MASHIRIKA YA KIRAIA NA SEKTA BINAFSI**

Hatua ya Rais Dkt. Mwinyi kuipa mashiko dhana hiyo ngeni kwa Tanzania visiwani, imechambuliwa na wasomi katika kuonesha umuhimu wa uchumi wa buluu hasa kwa maeneo yaliyozungukwa na bahari, maziwa na mito.

Wachambuzi wa mambo wanaamini kuwa takriban asilimia 40 ya watu duniani wanaishi karibu na bahari.

Kwa kuzingatia hilo kumekuwa na jitihada mbalimbali za kuimarisha uchumi endelevu unaotegemea bahari kwa kusimamia mifumo ya ikolojia ya pwani.

Miongoni mwa jitihada hizo ni kufanyika kwa mkutano wa Umoja wa Mataifa wa bahari uliofanyika mjini Lisbon nchini Ureno.

Mtaalamu wa masuala ya kimataifa ambaye pia ni Mhadhiri wa chou cha Diplomasia nchini, aBBAS Mwalimu alilieleza jarida hili kuwa idadi kubwa ya wananchi waishio pwani wanachangia kwakiasi kikubwa katika uchumi wa dunia kwa takriban dola trilioni 1.5 kwa mwaka huku matarajio yakionesha itaongezeka na kufikia takriban dola trilioni 3 ifikapo mwaka 2030.

"Uhakikishaji wa mfumo wa ikolojia ya bahari wenye afya utasaidia maisha ya wananchi na kukuza ukuaji wa uchumi, lakini kunahitaji usaidizi unaolenga sekta muhimu, ikiwa ni pamoja na uvuvi na ufugaji wa samaki, utalii, nishati, shughuli za meli na bandari, na uchimbaji wa madini ya baharini, pamoja na maeneo ya ubunifu kama vile nishati mbadala na teknolojia ya baharini.

## RASILIMALI ZA BAHARINI

Hii ni muhimu hasa kwa mataifa ya visiwa vidogo vinavyoendelea (SIDS), ambavyo rasilimali za baharini ni rasilimali muhimu, zinazowapa uhakika wa chakula, lishe, ajira, fedha za kigeni na burudani.



RAIS WA ZANZIBAR, DKT. HUSSEIN MWINYI.

Zaidi ya hayo, kupitia uingiliaji kati wa sera unaotegemea ushahidi, mali hizi zinaweza pia kutoa michango iliyoimarishwa na endelevu katika ukuaji wa uchumi, na ustawi wa SIDS na nchi zilizoendelea duniani (LDCs).

Kwa upande wake Profesa Hadley Mafwenga alilieleza jarid hili kuwa uchumi wa buluu ni muhimu sana kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, kwani eneo hilo limebeba uchumi endelevu.

"Ni kweli mabadiliko ya tabianchi yanaendelea kuathiri dunia, lakini ipo haja kwa jumuiya za kimataifa kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Zanzibar kwenye eneo la uchumi wa buluu ambao ni muhimu kwa maisha ya watu nan chi kwa ujumla.

"Ninaona wawekezaji wanakuja na ninaamini ni muhimu sana kwamba, kimataifa, tuendelee kuzingatia, ili tuweze kujenga ushirikiano kati ya mashirika ya kiraia na sekta binafsi," alisema.

## UCHUMI WA BULUU ENDELEVU NI NINI?

Mchumi mbobevu na mwanasiasa nguli nchini, Profesa Ibrahim Lipumba, aliliambia jarida hili kuwa licha ya kukosekana kwa ufafanuzi unaokubalika na wote wa neno uchumi wa buluu, Benki ya Dunia inafafanua kama matumizi endelevu ya rasilimali za bahari kwa ukuaji wa uchumi, kuboresha maisha, na kazi wakati wa kuhifadhi afya ya mfumo ikolojia wa bahari.

"Uchumi wa buluu unatanguliza nguzo zote tatu za uendelevu: mazingira, kiuchumi na kijamii. Wakati wa kuzungumza juu ya maendeleo endelevu, ni muhimu kuelewa tofauti kati ya uchumi wa buluu na uchumi wa bahari.

"Neno hili linamaanisha kuwa mpango huo ni endelevu wa mazingira, unajumuisha na unastahimili tabianchi. Pamoja na kutoa bidhaa na huduma zinazoweza kupimika kwa njia za fedha, miamba ya matumbawe, mikoko, nyasi bahari na ardhioevu, hutoa huduma muhimu za mfumo ikolojia kama vile ulinzi wa pwani na uondoaji kaboni."

Prof. Lipumba alifafanua kuwa nchi za visiwa vidogo zinazoendelea zinadhibiti asilimia 30 ya bahari na bahari zote. "Lakini je, SIDS na sekta binafsi zinawezaje kujenga ubia sawa na unaowajibika kwa ajili ya bahari endelevu, wanapaswa kutoa wito wa utekelezaji wa ahadi zilizoainishwa katika Mfumo wa Utekelezaji wa haraka wa SIDS, unaojulikana kwa njia fupi ya SAMOA Pathway na matarajio ya Lengo namba 14 la Maendeleo Endelevu (SDG14), kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya bahari.

Aidha alisisitiza kuwa ni muhimu kushirikisha sekta binafsi katika kulifanikisha dhamira ya kuleta maendeleo kupitia uchumi wa buluu.

## USHIRIKI WA WANAWAKE

Mwenyekiti wa chama cha Wanahabari wanawake (TAMWA), Joyce Shebe aliliambia jarida hili kuwa mpango madhubuti wa utekelezaji unahitajika, pamoja na uwepo wa sheria.

WASOMI

WAUCHAMBUA UCHUMI WA

# BULUU

"Tunahitaji kuona wanawake kama sehemu ya uchumi wa buluu, tunahitaji kuwaona kila mahali, ili kuingiza ushiriki wao, kwa sababu bila uongozi wao, ubinadamu kwa ujumla utapoteza mengi." Imewekwa wazi pamoja na mambo mengine bado ushiriki wa kada zote unahitajika wakiwemo watetezi wa mazingira, viongozi wa dunia, wafanyabiashara, vijana, washawishi, na wanasayansi ili kuendelea kuwasha msukumo mpya wa kuendeleza SDG14, katika lengo kuu la kutaka hatua ya kimataifa ya kulinda maisha chini ya maji.

Hatua madhubuti zitachukuliwa ili kujenga ustahimilivu wa bahari na jumuiya endelevu zaidi, zikiungwa mkono na wimbi jipya la ahadi za kurejesha afya ya bahari.

### UNAJUA NINI KUHUSU UCHUMI WA BULUU

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu, Zanzibar, Dkt. Aboud Jumbe alisema Uchumi wa Buluu ni shughuli za kiuchumi zinazohusu matumizi bora ya rasilimali za bahari kwa ajili ya kuimarisha au kukuza uchumi.

Zanzibar, kwa mfano sekta ya uvuvi huchangia 2.6% ya pato ghafi la Zanzibar, hutoa ajira za moja kwa moja kwa watu 200,000 wakati zaidi ya watu laki 4 hutegemea sekta hii.

Kuna nafasi kubwa na nzuri ya kuifanya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kuwa na uchumi mzuri zaidi kwa kuifanyia maarifa zaidi Blue Economy.

Imeelezwa yapo maeneo ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi zaidi kwani kiasi cha dola za Kimarekani Billion 23 hupotea kwenye uchumi wa dunia kila mwaka kwa uvuvi haramu.

Zaidi ya aina million 2.2 za wanyama, mimea na wanyama wengine huishi baharini

Asilimia 2 ya wanawake duniani hujihusisha na shughuli za bahari

Watu Billion 3.1 huishi ndani ya km 100 kutoka baharini.

Asilimia 90 ya biashara yote duniani hupitia baharini na inaongezeka maradufu kufikia 2030.

Bahari na uchumi endelevu wa bahari ni kiini cha uchumi wa kileo.



ASILIMIA

90

YA BIASHARA YOTE DUNIANI HUPITIA BAHARINI NA INAONGEZEKA MARADUFU KUFIKIA 2030.

KUTOKA KWA

# Mhariri Mtendaji

## UCHUMI WA ZANZIBAR KATIKA MIKONO SALAMA

UNAPOTAJA neno uchumi wa Buluu kwa sasa, haraka fikra zitakimbilia visiwani Zanzibar, na moja kwa moja taswira ya Rais wa visiwa hivyo Dkt. Hussein Ali Mwinyi itakujia.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, yeye ndie mwasisi wa dhana hiyo mpya ya kiuchumi Zanzibar.

Ni yeye ndie mwenye kuweza kuizungumza vizuri dhana hiyo kuliko mtu mwengine yeyote, ukweli wa hilo umeshuhudiwa na jarida hili baada ya kukutana nae visiwani Zanzibar.

Dkt. Mwinyi ameamua kuuweka uchumi wa Zanzibar kwenye mikono salama ya wananchi wenyewe wa visiwa hivyo.

Amefanya hivyo kwa sababu ya kutambua wazi kuwa ardhi ya Zanzibar ni ndogo, kwa kiasi kikubwa visiwa hivyo vimezungukwa na bahari, hivyo basi njia pekee na salama ya kuwa na uchumi shirikishi ni kuitumia bahari na rasilimali zake katika kuinufaisha nchi na mwananchi mmoja mmoja.

Dhamira yake hii inamfanya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, sasa kutazamwa kama mbeba maono wa maendeleo endelevu ya Zanzibar na pengine Tanzania kwa ujumla.
Mwenendo wake wa kiutendaji tangu alipoingia madarakani mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 25, 2020, unalifanya jarida hili, kuamini kuwa uchumi wa visiwa hivyo uko kwenye mikono salama.
Rais Dkt. Mwinyi amekuwa kinara wa harakati za maendeleo na katika kudhihirisha hilo ameamua kuitumia Bahari kuwa kimbilio la wengi.
Uchumi wa Buluu (Blue Economy) ni uchumi unaohusisha shughuli zote za ndani na nje ya eneo la bahari kwa maana ya fukwe na maji yenyewe, tunaamini hatua hii itasaidia kuwaondoa vijana wengi mtaani na kuwaingiza baharini katika kujitafutia ridhiki halali.

Tunaamini uamuzi wake huu ndio unaomfanya kiongozi huyu mwenye kutenda zaidi ya kusema kutazamwa kama Rais mbeba maono aliyeamua kuuweka uchumi wa visiwa hivyo kwa wananchi wote bila kujali jinsia zao.

Jarida hili linamuunga mkono na kuahidi kushirikiana nae katika kuisemea dhana ya uchumi wa Buluu kama alivyowahi kutoa ombi hilo yeye mwenyewe Machi 9,2022 visiwani Zanzibar.

Tunaamini sisi kama chombo cha Habari tunao wajibu wa kushiriki kwa namna moja ama nyengine kuzungusha pamoja gurudumu la maendeleo ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu bariki dhana ya uchumi wa buluu ifanikiwe kwa kiwango cha juu.



Jimmy C. Kiango
MHARIRI MTENDAJI



TIPER BULK STORAGE
VISION PLUS EYE CLINIC
TIB CORPORATE BANK Your Partner Bank
KCB BANK
Air Tanzania The Wings of Kilimanjaro
CRDB BANK Tunakusikiliza
NSSF Board of Trustees National Social Security Fund

# SHUKRANI
za dhati kwa WASHIRIKA WETU




# Experience the power of TemboCARD

Shop locally and internationally at over 44 million merchants and 2 million ATMs

VISA

CRDB BANK

*The bank that listens*